**HABARI FUPI**

## Vijana

Mpango wa shughuli za Vijana umebadilika kiasi baada ya kufunga kazi zote mwezi wa nne. Hata hivyo, viongozi wa Dekania ya Ng'arua walikutana mwezi wa sita kupanga upya utaratibu wao. Vile vile, viongozi wa vijana wa Parokia, watano kutoka kila Kanisa, watakutana Jumamosi 17 Julai jioni, Ol Moran kwa kutengeneza mpango wa kiparokia.
Nafasi ya kwanza ijayo ya Vijana wa Dekania ya Ng'arua kukutana pamoja itakuwa siku ya michezo (Ball Games), Jumamosi 28 Agosti, Sipili.
Zaidi ya hayo, katika kila Kanisa Dogo, vijana waendelea kukutana na kuwa na shughuli za kikanisa.

## Choir

Wanakwaya wanaendelea na mazoezi ya nyimbo za ibada.
Tena, hivi karibuni wataanza kujiandaa kwa mashindano ya nyimbo ya Dekania ya Ng'arua, yatakayofanywa mwezi wa kumi.

## Vyama

**CA** - Wanachama wote wa CA ya Jimbo watakuwa pamoja kule Nyahururu Jumamosi 17 Julai kwa kumtembelea Baba Askofu Joseph.

**CWA** - Akina Mama wa CWA wa Parokia watawatembelea Masista wapya watakaokuja Ol Moran Jumapili 11 Julai.
Kisha, kutakuwa na siku ya CWA kuwatembelea Mapadri wa Dekania ya Ng'arua, kule Kinamba, Ijumaa 23 Julai.

**CMA** - Chama kitakuwa na siku ya maombi ya kitaifa Jumapili 22 Agosti katika Kanisa Kuu la Ngong.
Wanachama wa CMA wa Parokia walifanya upya Nadhiri zao Jumatano 26 Mei kule Mithuri.
Waakilishi wa CMA kutoka kila Parokia ya Dekania ya Ng'arua walikutana kwetu Ol Moran Jumamosi 18 Juni kwa siku ya kazi ya huruma (*Charitable Day*). Baada ya Misa kanisani, walikwenda kuwatembelea watoto wa *Magnificat* na wanafunzi wa *Special Unit* ya Ol Moran, na kuwapatia msaada wao.



## Padri na Mashemasi Wapya wa Jimbo



Jumamosi 8 Mei, Njabini, Askofu Joseph aliweka wakfu kwa ajili ya Jimbo la Nyahururu:

**Shemasi James Ndirangu Ndiritu** kutoka Muhotetu, akatumwa Weru;

**Shemasi Henry Ndemi Njuguna** kutoka Dundori, akatumwa Kanyagia;

**Padri Samuel Kimajara Maina** kutoka Njabini, akatumwa Dundori.

## Uzinduzi wa Nyumba ya Maaskofu

Jimbo la Nyahururu lilikuwa na sherehe kubwa kwa ajili ya uzinduzi na baraka ya nyumba mpya ya Baba Askofu, kule Nyahururu, Runda Estate, Jumamosi 3 Julai. Mradi huu umekamilika kwa msaada wa wafadhili na pia kwa mchango wa kila Parokia ya Jimbo.
Sherehe ilianza na Misa ya Shukrani, iliyoongozwa na Kadinali John Njue, Askofu Mkuu Mstaafu wa Nairobi, pamoja na Askofu wetu Joseph Mbatia, Askofu Mstaafu Luigi Paiaro, na Maaskofu wengine na Mapadri wa Jimbo. Sherehe ilihudhuriwa pia na Watawa, viongozi kadhaa wa Serikali, tena waakilishi wa Wakristu wa kila Parokia.



### Utaratibu wa Julai—Agosti 2021

Jumapili 11 Julai - ya 15 ya kipindi cha Mwaka *(Mk 6:7-13)*
→ Misa - 9am: Ol Motunyi, Kahuho, Miharati; 11am: Ngoisusu, Ol Moran

Ijumaa 16—Jumamosi 17 Julai
→ 6.00pm: Ol Moran, Junior Catechists Training ya kiparokia

Jumamosi 17 Julai
→ 7.00pm: Ol Moran, Youth Council, viongozi watano wa vijana kutoka kila Kanisa Dogo

Jumapili 18 Julai - ya 16 ya kipindi cha Mwaka *(Mk 6:30-34)*
→ Misa - 9am: Minjore, Mithuri, Dam Mbili; 10.30am: Ndunyuriwo; 11am: Ol Moran; 12noon: Nakwam

Jumamosi 24 Julai
→ 10.00am: Ol Moran, Arusi ya Martin Kamore na Mary Nyagaki

Jumapili 25 Julai - ya 17 ya kipindi cha Mwaka *(Yoh 6:1-15)*
→ Misa - 7am: Kabati; 8am: Survey; 9am: Githima, Mbombo; 10am: Naibor; 11am: Ol Moran; 12noon: Posta

Jumapili 1 Agosti - ya 18 ya kipindi cha Mwaka *(Yoh 6:24-35)*
→ Misa - 9am: Magadi, Gituamba, Ngare Narok; 11am: Ol Moran, Lounyek

Jumamosi 7 Agosti
→ 10.00am: Ol Moran, Mkutano wa Makatekista wote

Jumapili 8 Agosti - ya 19 ya kipindi cha Mwaka *(Yoh 6:41-51)*
→ Misa - 9am: Ol Motunyi, Kahuho, Miharati; 11am: Ngoisusu, Ol Moran

## Sakramenti ya Kitubio

Kila Jumamosi, kuanzia saa tisa, Kanisani Ol Moran, Padri mmoja yupo tayari kwa ajili ya Sakramenti ya Kitubio cha Wakristu.
Katika Makanisa Madogo, Sakramenti ya Kitubio huweza kupokelewa kabla ya Ibada ya Misa ya Jumapili.
Ni msaada mkubwa katika maisha ya Kikristu kuzoea kufanya Kitubio mara kwa mara, kusamehewa dhambi na kutafuta utakatifu.

SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO
*- No. 82, Year 13, Printed on 10th July 2021 - (NOT FOR SALE)*
**SAINT MARK** CATHOLIC PARISH - Ol Moran - *Catholic Diocese of Nyahururu*
*P.O.Box 20 - 20320 Kinamba* - saintmark@olmoran.it - +254 720 924 153

**Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia**
*Aliishi Yerusalemu. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Kisha aliishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Akawa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.*

**Gazeti la Parokia Katoliki ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran**
*N. 82 — Mwaka wa 13*
**Julai 2021**

# SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO

*Mwaka Maalum wa Mtakatifu Yosefu, Mume wa Bikira Maria*

## Mwenye haki, safi, mtiifu

Kuwa mjanja, kujipanga kivyako, kukalia wengine na hata kuwadanganya, ikiwezekana. Hivyo lazima ufanye ukitaka kufaulu katika dunia hii. Na hiyo ndiyo ile dunia tuliyotengeneza.

Ikiwa hivyo ni kweli, mtu kama Yosefu wa Nazareti angekuwa mtu wa kisasa, au yuko nje ya dunia? Fadhila zake zingemsaidia? Kuwa mwenye haki, badala ya udanganyifu; kuwa safi, badala ya ujanja; kuwa mtiifu, badala ya ubinafsi: siku hizi yafaa kweli?

Papa Fransisko ametaja mwaka huu 2021, kwa ajili ya Kanisa lote, kuwa Mwaka Maalum wa Mtakatifu Yosefu, baba mlezi wa Yesu Kristu, mume wa Bikira Maria, mlinzi wa Famili Takatifu, Msimamizi wa Kanisa Katoliki.

Je, una maana gani mwaka huu maalum? Papa Fransisko ametualika kukumbuka na kutazama mfano wa Mtakatifu Yosefu hasa kwa sababu ya fadhila zake za pekee. Kama tunavyosoma hasa katika Injili za Mathayo na Luka, Yosefu alijulikana kuwa mtu mwenye haki, safi na mtiifu. Hakuwa mzee wa kutoa tu amri zake kwa boma, bali mtu tayari kusikia mapenzi ya Bwana na kuyafanya. Mtu wa haki, aliyemheshimu bibi yake na mtoto wake, safi katika nia na katika vitendo vyake pia. Hapo Yosefu ameiga mfano wa Kristu mwenyewe, aliyekuja kutimiza mapenzi ya Mungu Baba.

> Fadhila zake zatufaa sisi watu wa wakati huu? Ama tunataka dunia ya aina gani? Tutafakari...


Fadhila zake zinaweza kusaidia Kanisa, familia zetu na jamii za siku hizi? Kuwa watu wa haki, kuwajali wengine na nia safi, kutii amri za Mungu kwafaa vipi katika dunia ya siku hizi?

Basi, na tufanye bidii kutengeneza dunia tofauti, ama angalau Kanisa jipya, na familia zetu, angalau mioyo yetu!

Yosefu ni Mtakatifu Msimamizi wa Kanisa lote pia. Katika Makanisa yetu, Jumuiya na vikundi, tuendelee kutafakari ujumbe wake, katika Biblia na katika maombi, hadi fadhila zake ziingie katika mwenendo wetu.

Fr. Giacomo Basso - *Baba Paroko*

Mtakatifu Yosefu, Baba mlezi wa Yesu.



## MIITO: MASISTA WAPYA KUMI

*Jumamosi 26 Juni, kule Nairobi, Masista wetu wa Shirika la 'Servants of the Visitation' walipokea baraka ya Masista wapya kumi waliofanya Nadhiri za kwanza za Utawa. Ibada ya Misa ya Nadhiri iliongozwa na Baba Askofu wa Nyahururu, Joseph Mbatia.*

*Masista Wapya ni Ana Maria Da Rocha (kutoka Brazil), Elizabeth Mbuli Ndaka (Machakos), Gertrude Bonareri Nyangau (Kisii), Holitiana Marie Flavie Rahanitriniaina (Madagascar), Jane Njoki Muthee (Sipili), Josephine Gesare Obiri (Kisii), Lydhia Wanjiru Ngigi (Mochongoi), Marie Perline Razanadravao (Madagascar), Marie Thérèse Rasoanivo (Madagascar), Volatiana Marie Louisette Razafindravao (Madagascar). Watakuja Ol Moran kusalimia Wakristu Jumapili 11 Julai.*

*Walisimamiwa na Sista Mkuu wa Shirika, Sr. Maddalena Ergasti. Sista Mkuu alitembelea hata Parokiani kwetu Ol Moran siku zilizotangulia sherehe, kuona kazi za Masista na kupanga uteuzi wao.*

*Kitabu cha Sala kwa Mtakatifu Yosefu, Ng'arua Deanery*


## NENDENI KWA YOSEFU

*Katika Dekania ya Ng'arua kimetolewa kitabu cha mafunzo na maombi kwa ajili ya Mwaka Maalum wa Mtakatifu Yosefu, kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza pia.*

*Kinaweza saidia katika Jumuiya Ndogo Ndogo, au kwenye vikundi na vyama, na pia kwa ajili ya maombi ya mtu binafsi.*

*Vitabu vinauzwa katika kila Parokia.*

***KShs 50/=***





*Uteuzi wa Makatekista na Makanisa Mapya*

# Huduma muhimu ya Makatekista

SHEREHE YA UTEUZI - Vijilia ya Pentekoste, Jumamosi 22 Mei, Makatekista wote walikusanyika Kanisani Ol Moran kwa ajili ya Misa na Baraka ya Uteuzi. Wakahudhuria ibada hata wanachama wa Halmashauri Kuu na Waratibu wa kila Kanisa Dogo. Makatekista pamoja na Wasaidizi *(Assistant Catechists)* wakaomba pamoja nguvu ya Roho Mtakatifu kwa sababu ya huduma yao, na waliombewa baraka maalum. Kisha Makatekista wakapewa barua ya uteuzi wa mwaka huu, na wakapokea ishara ya Msalaba.

MAKATEKISTA WAZEE - Katika hiyo sherehe, Makatekista wazee walioendelea katika huduma kwa miaka mingi, walitambuliwa na Makatekista wote kwa sababu ya kazi zao nyingi, na kupewa zawadi ya shukrani.

MAKANISA MAPYA - Katika kuwatuma Makatekista, Mapadri walijaribu kushughulikia hata yale Makanisa mapya yanayofunguliwa wakati huu, hasa Kanisa la Ngoisusu na Naibor. Ngoisusu Wakristu na watu wa eneo washaanza kukutana siku ya Jumapili. Pia, wazazi wa eneo hilo wameanza kupanga masomo ya shule ya watoto wadogo katika shamba la Kanisa. Jumapili 11 Julai kutakuwa na Misa ya kwanza kule baada ya miaka mingi: kwa kweli Ngoisusu kulikuwa na Kanisa kitambo, likabomolewa wakati wa vita vya kikabila. Naibor pia, Kanisa Dogo limeanza katika shule ya msingi 'Naibor Amani'.

JUNIOR CATECHISTS - Jumamosi 19 Juni yalianza masomo ya 'Junior Catechists', yaani mafunzo kwa ajili ya Makatekista Wapya. Mwaka huu masomo yataendelea katika Parokia, na pia katika Dekania ya Ng'arua. Parokia tano za Ng'arua Deanery zimepanga kuwa na masomo pamoja kwa ajili ya Makatekista Mapya. Mkutano ujao wa Junior Catechists wa Parokia utakuwa Ijumaa 16 na Jumamosi 17 Julai. Masomo ya Dekania yataanza hapa Ol Moran tarehe 12-14 Agosti.

*Juu:* Makatekista wakipewa ishara ya Msalaba wa Uteuzi.

*Chini kushoto*: Kikundi cha Makatekista.

*Chini kulia*: Makatekista Wazee waliosherehekewa.





*PMC Baraka Day na Mashindano*

# Watoto wa Kanisa!

Watoto wa PMC walifanya Harambee Jumapili 6 Juni, ili kuchangia kazi za watoto Parokiani, pia mradi wa Jimbo la Nyahururu wa mwaka huu. Walikutana wote pamoja Ol Moran, katika ibada ya Sherehe ya Mwili na Damu ya Kristu, iliyofanywa nje, nyuma ya Kanisa. Baada ya Misa na nafasi ya kuabudu Ekaristi, watoto na Promoters waliendelea kuleta pamoja michango yao, hata kutoka Makanisa Madogo. Pia Wakristu na wageni waliwasaidia.

Tena, watoto walikutana Ol Moran Jumamosi 12 Juni kwa sababu ya mashindano ya nyimbo kati ya Makanisa Madogo ya Parokia. Siku ikawa yenye furaha, na hayo ni matokeo ya mashindano:

- Singing Game: 1) St. Charles Lwanga Zone; 2) St. Maria Goretti Zone; 3) Githima-Gituamba Team; 4) St. Michael Zone.
- Dance: 1) St. Maria Goretti Zone; 2) St. Charles Lwanga Zone; 3) St. Michael Zone.
- Choral Verse:1) St. Charles Lwanga Zone; 2) St. Maria Goretti Zone.
- Over All: 1) St. Charles Lwanga Zone; 2) St. Maria Goretti Zone; 3) St. Michael Zone.



*Juu:* PMC Baraka Day, wakati wa mchango, Jumapili 6 Juni.

*Kushoto:* Mashindano ya nyimbo za PMC, Jumamosi 12 Juni.



*Lami ya barabara kuu*

# Palipo na moshi, kunao moto?

*Hilo si swali baya: ni vile haijakuwa rahisi kuamini macho yetu! Baada ya miaka mingi ya ahadi na maneno, matendo yameanza kuonekana. Barabara kuu ya Ol Moran hadi Mahiga inafanywa lami. Je, lami itafika kwetu kweli? Kazi itaenda mbio? Barabara mpya itaelekea wapi? Haya ni kati ya maswali ambayo wenyeji wajiuliza sana. Alhamisi 1 Julai mbunge wa Laikipia North Sara Lekorere pamoja na mbunge wa Laikipia West Patrick Mariru waliwaelezea raia mradi huu katika baraza hapa Ol Moran. Kazi imekabidhiwa kwa 'Debroso Construction Co. Ltd.', kutoka Nairobi, na imeshaanza pande ya Mahiga.*

*Hapo hivi lazima pia tutambue bidii ya kufanya ukarabati wa barabara nyingi za ndani ndani, mwaka huu hasa katika eneo la Sosian: zimetengenezwa barabara za Ol Moran kuelekea Miharati, Survey, Magadi mpaka Lounyek, tena Dam Samaki, pia Kahuho, Mutarakwa na Githima.*

*Chini:* Barabara kuu Ol Moran - Sipili, inapofika lami kule Mahiga.



*Padri Mstaafu Parokiani*

# Fr. Victor amekaribishwa

Anaitwa Padri Vittorio Grigoletto, ama Fr. Victor, naye ni Padri mzee aliyekuja, mwisho wa mwezi wa tano, kukaa Ol Moran pamoja na Mapadri wa Parokia. Alitoka Jimbo la Padua, kule Italia, akatumwa Kenya mwaka 1978. Tangu mwaka ule, alifanya kazi katika Parokia kadhaa za eneo la Nyandarua, katika Jimbo la Nyahururu. Alipofikia umri wa miaka 75, akapewa ustaafu na kutumwa Parokiani mwetu. Hata hivyo, bado ana nguvu na moyo wa kuendelea na kazi, atasaidiana na Mapadri wa Parokia kwa ajili ya huduma ya Wakristu.



*Juu:* Fr. Victor pamoja na Fr. Simon na Watumishi wa Altare.

**Rev. Fr. Vittorio Grigoletto**

*1945 - Born in Italy, Padua.*
*1971 - Priestly Ordination.*
*1978 - Sent to Kenya as a 'Fidei Donum' Missionary, to the Diocese of Nyeri, then Nyahururu.*

*Main Pastoral Services:*
*1978 - Parish Assistant at Nyahururu.*
*1983 - Parish Priest of Ol Kalou.*
*1988 - First Parish Priest of Ol Joro Orok.*
*2003 - First Parish Priest of Murungaru.*
*2011 - First Parish Priest of Weru.*
*2021, May - Retired and assistant at Saint Mark Catholic Parish of Ol Moran.*





*Maendeleo ya Tumaini na Hekima*

# Yote kwa ajili ya Elimu Bora

TUMAINI BOARDING - Shule ya Msingi ya Parokia 'Tumaini Academy' imeweza kupata usajili mpya wa Wizara ya Elimu kama shule ya msingi *"Mixed Day & Boarding"*. Hatua hii imefaulu kwa sababu ya mijengo ya mabweni inayoendelea.

UZINDUZI WA BWENI - Bweni la kwanza kwa ajili ya wasichana umekamilika, na wanafunzi wameshaingia. Alhamisi 1 Julai kulikuwa na sherehe yenye furaha kwa ajili ya uzinduzi wa bweni lililokamilika, pia baraka ya jiwe la kwanza la bweni la wavulana na la chumba kikuu cha shule, zilizoanza kujengwa. Misa iliongozwa na Fr. Peter Kinyua, aliyebariki mjengo mpya. Kisha Fr. Simon alibariki na kulaza jiwe la kwanza la bweni la wavulana, na Fr. Vittorio alibariki jiwe la kwanza la darasa kuu. Fr. Giacomo aliwaelezea wazazi na wageni mpango wa mradi na kuwashukuru wafadhili.

IN-TAKE - Kuanzia juma lililopita, wanafunzi wapya waweza kujiandikisha katika Nyumba ya Wanafunzi 'Hekima House', pia katika Shule ya Msingi Tumaini Academy, kwa masomo na vile vile kwa mabweni.

WAZAZI WA HEKIMA - Mkutano wa wazazi wa Hekima House ulifanyika Alhamisi 17 Juni, ili kuzumgumza kuhusu maisha na changamoto za wanafunzi, na kuhusu mpangilio wa Nyumba pia.

HEKIMA & TUMAINI STAFF - Walimu wa Tumaini na Hekima pamoja walikuwa na siku ya masomo yao Ijumaa 4 Juni, kwenye Parokia ya Marmanet. Baba Paroko Fr. Simon Mwai aliwakaribisha na kuwaongoza katika ibada ya Misa. Kisha wakaendelea kusoma pamoja na Fr. Giacomo kuhusu umuhimu wa elimu bora.

*Kushoto juu:* Walimu wa Tumaini na Hekima kule Marmanet.

*Kushoto chini:* Wasichana wa Tumaini kwenye bweni jipya.

*Chini:* Sherehe ya uzinduzi wa bweni la kwanza la Tumaini Academy.

